JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHERIA NA. 27 YA 1967 (SURA NA. 52)

# KANUNI ZA SHERIA YA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA
TOLEO LA 2019

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 11 cha Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa, Sura Na. 52)*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 393 la tarehe 10/5/2019

SHERIA YA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA
(SURA YA 52)

# KANUNI

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 11 cha Sheria)*

KANUNI ZA SHERIA YA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA, 2019

## MPANGILIO WA VIFUNGU

SEHEMU YA KWANZA

MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MADHUMUNI YA KANUNI

4. Madhumuni ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIAJI WA MATUMIZI NA MAENDELEO YA KISWAHILI

5. Dhamira kuu.
6. Kanzidata ya Wataalamu wa Kiswahili.
7. Utaratibu katika kusanifisha istilahi za Kiswahili.

SEHEMU YA NNE
MAFUNZO YA KISWAHILI KWA WAGENI

8. Baraza kusimamia mafunzo ya Kiswahili kwa wageni.
9. Utaratibu wa kupata Cheti cha Utambuzi.

10. Baraza kuthibitisha mtaala na vitabu vya kufundishia.
11. Mikutano ya Baraza na wamiliki wa vituo.
12. Kuendesha mafunzo bila cheti cha utambuzi ni kosa.
13. Cheti cha kufuzu.
14. Baraza kufuatilia mafunzo na kushauri vituo.
15. Utaratibu katika kufuatilia mafunzo.

SEHEMU YA TANO
MATAMASHA NA MASHINDANO YA KISWAHILI

16. Baraza kusimamia na kutoa Idhini ya matamasha au mashindano yanayohusisha Kiswahili.
17. Maombi ya Idhini ya kufanya matamasha au mashindano.
18. Usalama wakati wa tamasha au shindano.
19. Kanuni za mashindano kuwasilishwa Baraza.

SEHEMU YA SITA
HUDUMA ZA BARAZA KWA VYOMBO VINGINE

20. Baraza kuhamasisha na kuelimisha matumizi sahihi ya Kiswahili.
21. Baraza kutoa ushauri
22. Utaratibu wa kupata tafsiri kutoka Baraza.
23. Baraza kuhariri miswada ya kazi za Sanaa.
24. Kuimarisha uhariri katika vyombo vya habari.
25. Utaratibu wa kupata tafsiri rasmi.
26. Mafunzo maalumu kwa wanahabari.
27. Baraza kusahihisha makosa ya lugha katika vyombo vya habari.
28. Matangazo ya biashara kuhakikiwa.
29. Matangazo ya dharura au maafa

SEHEMU YA SABA
HUDUMA ZA BARAZA KWA UMMA

30. Baraza kutoa huduma ya ushauri.
31. Huduma zinazotolewa na Baraza.
32. Utaratibu wa kupata huduma za uhariri, tafsiri, kuhakiki na kutoa ithibati.
33. Utaratibu wa kupata huduma ya ukalimani.
34. Baraza kusimamia ukalimani wa lugha ya alama.
35. Kanzidata ya wakalimani na wataalamu wa lugha ya alama.
36. Utaratibu wa kupata mkalimani wa lugha ya alama.

SEHEMU YA NANE
KISWAHILI KUTUMIKA KAMA BIDHAA

37. Wajibu wa Baraza katika ubidhaishaji wa Kiswahili
38. Huduma za Kiswahili.
39. Utaratibu wa kupata idhini ya kutoa huduma zinazohusisha Kiswahili.
40. Ufuatiliaji na tathmini.

SEHEMU YA TISA
UTAFITI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

41. Idhini ya utafiti kutolewa na Baraza.
42. Taarifa au takwimu zilizo katika Baraza.

SEHEMU YA KUMI
UANDISHI WA VITABU NA ITHIBATI

43. Baraza kuhamasisha waandishi chipukizi.
44. Vitabu vya kiada na ziada kuthibitishwa.
45. Kusambaza kitabu kisicho na ithibati.
46. Wahariri binafsi kutumika.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
KISWAHILI KATIKA BIDHAA NA MAZINGIRA YA VIWANDA

47. Baraza kufuatilia matumizi ya Kiswahili katika bidhaa za viwandani.
48. Elimu na uhamasishaji.
49. Wajibu wa kutumia Kiswahili na kutafsiri maelekezo kwenye bidhaa.
50. Utaratibu wa kuomba tafsiri au uhakiki wa lugha katika bidhaa.
51. Masharti ya mpito.

# SHERIA YA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (SURA YA 52)

## KANUNI

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 11 cha Sheria)*

KANUNI ZA SHERIA YA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA, 2019

### SEHEMU YA KWANZA MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa za Mwaka 2019, na zitaanza kutumika tarehe ambayo zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika Tanzania Bara katika kuliwezesha Baraza kutekeleza majukumu yake kama yalivyotamkwa katika Sheria.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi tafsiri ya maneno muhimu itakuwa kama ifuatavyo:

"Baraza" maana yake ni Baraza la Kiswahili la Taifa ambalo kwa kifupi litaitwa "BAKITA"; lililoundwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria Namba 27 ya mwaka 1967;

"BASATA" maana yake ni Baraza la Sanaa la Taifa lililoundwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, Namba 23 ya mwaka 1984;

"Bodi ya Filamu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Namba 4 ya mwaka 1976 na marekebisho au mbadala wake;

"Cheti cha Utambuzi" maana yake ni hati mahususi inayotolewa na Baraza kwa ajili ya kutambua utaalamu wa mtu, kikundi au taasisi inayofanya shughuli inayohusisha Kiswahili;

"Kamisheni" maana yake ni Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayoshughulika na maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili;

"Katibu" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Baraza

aliyeteuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria;

"Idhini" maana yake ni hati mahususi inayotolewa na Baraza kwa ajili ya kuruhusu mtu, kikundi au taasisi kufanya shughuli inayohusisha Kiswahili;

"Lugha" maana yake ni chombo cha mawasiliano kinachotumia maneno, ishara na alama ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Pia, katika Kanuni hizi inahusisha lugha za alama;

"Lugha ya Taifa" maana yake ni Kiswahili;

"Mdau wa Kiswahili" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, asasi au chama chochote kilichosajiliwa kisheria kinachojishughulisha na maendeleo au matumizi ya lugha ya Kiswahili;

"Mfasiri" maana yake ni mtaalamu wa kutoa tafsiri kutoka au kwenda katika lugha ya Kiswahili;

"Mhariri" au "Mhakiki" maana yake ni mtu anayetathmini na kukagua uzingativu wa ufasaha na usanifu wa Kiswahili katika maandiko;

"Mratibu" maana yake ni ofisa aliyeteuliwa na Baraza chini ya kifungu cha 5 cha Sheria kuelekeza matumizi sahihi ya Kiswahili;

"Mtaalamu" maana yake ni mtu mwenye ujuzi wa kutekeleza jambo linalohusiana na uendelezaji au ukuzaji wa matumizi ya Kiswahili;

"Mtaalamu aliyethibitishwa" maana yake ni mtu mwenye cheti cha utambuzi wa ujuzi wa kutekeleza jambo linalohusiana na shughuli zinazotekelezwa na Baraza;

"Sekretarieti" maana yake ni watumishi wa Baraza walioajiriwa na Baraza chini ya kifungu cha 5 cha Sheria na kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za utumishi wa umma ili kulisaidia Baraza kutekeleza majukumu yake;

Sura ya 52

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa, Namba 27 ya 1967;

"Waziri" maana yake ni Waziri wa Wizara yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Utamaduni wa Taifa.

## SEHEMU YA PILI
## MADHUMUNI YA KANUNI

Madhumuni ya Kanuni hizi

4. Kanuni hizi zinatungwa kwa madhumuni ya kuliwezesha Baraza kutekeleza mambo yafuatayo:

(a) kusimamia shughuli za maendeleo na matumizi

fasaha ya Kiswahili sanifu nchini;

(b) kushirikiana na vyombo vingine vinavyojishughulisha na uendelezaji wa kiswahili na kusimamia kazi zao;

(c) kutoa tafsiri rasmi na kusanifisha istilahi za Kiswahili;

(d) kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha na kuzuia upotoshaji wake;

(e) kushirikiana na mamlaka za sekta zingine katika kuandaa istilahi za sekta husika;

(f) kubidhaisha Kiswahili na kutambua wadau wake;

(g) kufanya na kusimamia tafiti mbalimbali za Kiswahili;

(h) kutoa ushauri kwa waandishi au wafasiri wa vitabu au machapisho yanayoandikwa kwa Kiswahili;

(i) kutoa ithibati ya lugha kwa vitabu vya Kiswahili vya nyanja mbalimbali za elimu;

(j) kusimamia huduma za ukalimani wa lugha ya alama katika shughuli za Serikali na za umma;

(k) kufuatilia na kushauri kuhusu shughuli mbalimbali za kukuza na kuendeleza Kiswahili.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIAJI WA MATUMIZI NA MAENDELEO YA KISWAHILI

Dhamira kuu

5. Baraza litasanifu istilahi za Kiswahili katika nyanja mbalimbali za matumizi kwa dhamira ya kukuza na kuendeleza Kiswahili ili kifikie kuwa:

(a) Lugha yenye nguvu duniani;

(b) Lugha ya kufundishia nchini;

(c) Lugha ya Taifa inayotumiwa kwa ufasaha na kila Mtanzania; na

(d) Lugha rasmi ya mawasiliano katika biashara za kimataifa.

Kanzidata ya Wataalamu wa Kiswahili

6.-(1) Ili kutimiza azma ya kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini Baraza linaweza kushirikiana na wataalamu wa nyanja mbalimbali,vyama vya kitaaluma au mamlaka zingine za umma katika kuibua au kutambua na kusanifisha

istilahi zinazoibuka katika sekta mbalimbali kwenye jamii ili kuendeleza na kukuza matumizi ya Kiswahili.

(2) Baraza litaimarisha dhana ya ukuzaji na uendelezaji shirikishi wa Kiswahili kwa kutambua na kutunza kanzidata ya wataalamu na wadau wa Kiswahili; mtu binafsi, kikundi cha watu, vyama vya kitaaluma au asasi za kitaalamu zinazojishughulisha au kujihusisha na ufanikishaji wa mambo yanayochangia kukuza matumizi na kuendeleza Kiswahili zilizopo ndani na nje ya Tanzania Bara.

(3) Mtu binafsi, kikundi cha watu, asasi au chama cha kitaaluma kinaweza kutambuliwa na kuingizwa katika kanzidata ya Baraza kama mtaałamu au mdau wa Kiswahili kutokana na taaluma au shughuli kinazofanya baada ya kutimiza mambo yafuatayo:

(a) kujaza fomu ya maombi ya kutambuliwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Nane na kurejesha katika ofisi za Baraza kwa kutumia mfumo utakaoelekezwa na Baraza kwa wakati huo;

(b) kulipa Tozo ya maombi ya utambuzi kwa wataalam na wadau wa Kiswahili kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini;

(c) kupewa cheti cha utambuzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Tisa.

Utaratibu katika kusanifisha istilahi za Kiswahili

7.-(1) Usanifishaji wa Istilahi utafanyika kwa utaratibu ufuatao:

(a) kuchunguza na kukusanya maneno yanayoibuka katika jamii na yale yanayotokana na kukua kwa sayansi na teknolojia na ambayo hayana visawe vyake katika Kiswahili;

(b) kupokea mapendekezo ya istilahi kutoka kwa wadau mbalimbali wanaohitaji zisanifiwe kwa matumizi ya sekta husika;

(c) kusoma vitabu na katika mitandao mbalimbali kwa lengo la kukusanya maneno ya nyanja mbalimbali;

(d) kuhoji watu kuhusu maneno mbalimbali wanayoyatumia pasipo kupata Kiswahili chake;

(e) kuchunguza maneno yanayofanana na hayo kutoka katika lahaja mbalimbali za Kiswahili, lugha za Kibantu na lugha nyingine za Kiafrika.

(2) Baada ya Baraza kufanya yaliyoelezwa katika sehemu (1) litaandaa mapendekezo ya visawe na:

(a) kuitisha warsha ya wadau itakayohusisha wataalamu na wabobezi wa usanifishaji nchini pamoja na watendaji katika fani zilizowasilisha mapendekezo ya istilahi ili kujadiliana;
(b) kupokea maoni ya wadau;
(c) kuchapisha na kusambaza istilahi zilizosanifishwa kwa ajili ya matumizi ya umma;
(d) kufanya tathmini ya matumizi ya istilahi zilizosambazwa kwa watumiaji.

## SEHEMU YA NNE
## MAFUNZO YA KISWAHILI KWA WAGENI

Baraza kusimamia mafunzo ya Kiswahili kwa Wageni

8.-(1) Baraza litasimamia mafunzo ya Kiswahili kwa wageni yanayotolewa na wadau mbalimbali Tanzania Bara.

(2) Baraza litaanzisha vituo vya mfano vya kufundishia katika maeneo ambayo litaona inafaa kufanya hivyo.

(3) Baraza litatambua mtu, kikundi cha watu au asasi zinazomiliki vituo vya kufundishia Kiswahili kwa wageni kwa kutoa vyeti vya utambuzi.

(4) Cheti cha utambuzi chini ya kanuni hii kitatolewa mara moja tu wakati wa uhai wa mwombaji husika lakini kinaweza kufutwa na Baraza endapo mwombaji hatahuisha utambuzi huo kwa kipindi cha miezi 24 baada ya kuisha muda wake.

Utaratibu wa kupata Cheti cha Utambuzi wa kufundisha Kiswahili

9.-(1) Kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa Kanuni hizi katika Gazeti la Serikali, Baraza litatoa Cheti cha Utambuzi kwa mtu, kikundi cha watu au asasi iliyoanzisha au yenye nia ya kuanzisha kituo cha kufundishia Kiswahili kwa wageni.

(2) Ili kutambuliwa na kupata Cheti cha Utambuzi kwa ajili ya kufundisha Kiswahili kwa Wageni mwombaji atafuata utaratibu ufuatao:

(a) atajaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza katika Kanuni hizi;
(b) atalipa Tozo ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi;
(c) atarejesha fomu hiyo pamoja na viambatisho vilivyotajwa katika fomu hiyo kwa ofisa wa Baraza anayehusika kwa njia itakayokuwa imeelekezwa na Baraza;
(d) endapo mwombaji amekamilisha vigezo vya

kupewa Cheti cha Utambuzi atapaswa kulipa ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini na moja kwenye Kanuni hizi na kuwasilisha stakabadhi kwa Katibu wa Baraza na kukabidhiwa cheti husika.

(3) Muda wa kutumika kwa Cheti cha Utambuzi kilichotolewa na Baraza chini ya Kanuni hii ni miezi 12 tangu siku kilipotolewa na endapo mmiliki hata kihuisha kwa kipindi cha miezi 24 baada ya utambuzi wa awali kukoma Baraza linaweza kufuta utambuzi huo na mmiliki atalazimika kuomba kutambuliwa upya.

(4) Baada ya muda wa Cheti cha Utambuzi kumalizika mmiliki wa cheti hicho anaweza kuomba kukihuisha kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) atajaza fomu ya kuhuisha cheti hicho kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu katika Kanuni hizi na kuambatisha na cheti halisi kilichoisha muda wake;

(b) atalipa Tozo ya maombi kuhuisha cheti hicho kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi na kuambatisha stakabadhi halisi kwenye fomu ya maombi;

(c) atalipa ada ya kuhuisha cheti kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini na moja katika Kanuni hizi; na

(d) atarejesha fomu hiyo kwa Katibu wa Baraza kwa namna atakayoelekezwa wakati wa kupatiwa fomu husika.

(5) Vyeti vinavyotolewa na Baraza chini ya Kanuni hizi vitasainiwa na Katibu Mtendaji na kutiwa mhuri wa Baraza, muonekano wake utakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza kwenye Kanuni hizi.

(6) Mtu, kikundi au asasi inayoomba cheti cha utambuzi chini ya Kanuni hii itapaswa kwanza iwe imekamilisha taratibu zote za mamlaka zinazohusika kabla ya kuomba cheti cha utambuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni.

Baraza kuthibitisha mtaala na vitabu vya kufundishia

10.-(1) Baraza kwa kushirikiana na watoa huduma ya kufundisha Kiswahili kwa wageni litatoa ithibati kwa mtaala pamoja na vitabu vya kufundishia kwa ajili ya kuweka uwiano wa mafunzo hayo nchini.

(2) Mwombaji wa mara ya kwanza au anayehuisha

cheti atapaswa kuwa na mtaala na vitabu vya kufundishia vilivyothibitishwa na Baraza.

(3) Mtaala na vitabu vya kufundishia vitafanyiwa mapitio katika kila mkutano wa pamoja wa Baraza na wadau wanaotoa huduma hiyo, mkutano huo wa wadau utaamua pia bei elekezi ya mtaala na vitabu vinavyotumika katika huduma hiyo.

Mikutano ya Baraza na wamiliki wa vituo

11.-(1) Wamiliki na wadau wa vituo vya kufundishia Kiswahili nchini watakuwa na mikutano ya pamoja itakayoitishwa na Baraza ili kutathmini, pamoja na mambo mengine, ubora, changamoto na namna ya kukabili changamoto hizo katika huduma ya ufundishaji Kiswahili kwa wageni.

(2) Baraza litasimamia upatikanaji wa rasilimali za mkutano huo ambapo kila unapoitishwa utafanyika katika mkoa tofauti na awali na wajumbe wataazimia kuhusu mahali na namna ya kupata rasilimali za mkutano utakaofuata.

Kuendesha mafunzo ya Kiswahili bila ya kuwa na Cheti cha Utambuzi

12. Mtu, kikundi au asasi yoyote itakayobainika kuendesha mafunzo ya Kiswahili kwa wageni pasipo kupewa Cheti cha Utambuzi kutoka Baraza itakuwa inatenda kosa dhidi ya Kanuni hizi na Baraza linaweza kuchukua hatua zifuatazo:

(a) kumwandikia mmiliki wa kituo husika notisi ya kumtaka kufunga kituo au kufuata utaratibu wa kuomba Cheti cha Utambuzi katika Baraza ndani ya siku 30 tangu ilipobainika;

(b) kubandika matangazo au alama zozote za kukifunga kituo hicho endapo mmiliki husika hajatekeleza masharti ya kipengele (a), lakini matangazo hayo yanaweza kuondolewa ikiwa masharti yametekelezwa baada ya kufungwa kwa kituo husika; na

(c) kutaarifu mamlaka zingine za sheria ikiwa mmiliki amekaidi na hatua zilizochukuliwa na Baraza kwa kufunga kituo husika.

Cheti cha kufuzu

13.-(1) Mwanafunzi atapewa Cheti cha kufuzu baada ya kufanya na kufuzu majaribio ambayo yatapima uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika kwa Kiswahili kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne.

(2) Mwanafunzi atakuwa amefunzu kupata cheti cha

Baraza endapo atafikisha jumla ya alama 50 kati ya 100 kwenye majaribio aliyopewa.

(3) Ili kupata cheti mwanafunzi atalipa Tozo ya cheti kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

(4) Cheti kitakachotolewa kitakuwa na nembo ya Baraza pamoja na nembo ya kituo cha mafunzo alikohudhuria.

Baraza kufuatilia mafunzo na kushauri vituo

14.-(1) Baraza kwa kutumia watumishi au wataalamu waliotambuliwa chini ya Kanuni hizi litafanya ufuatiliaji na utoaji wa ushauri kwa wamiliki wa vituo ili kuimarisha ubora wa mafunzo na vituo vya kufundishia Kiswahili.

(2) Katika Kufuatilia ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni na ili kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa ubora unaostahili Baraza litakagua uzingatiaji wa mitaala iliyoidhinishwa, matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa, ubora wa mazingira ya kufundishia pamoja na kuchunguza sifa, tabia na uwezo wa walimu wanaotumika.

(3) Endapo kituo chochote kitakuwa na dosari yoyote katika mambo yaliyotajwa Baraza litachukua hatua zifuatazo:

(a) kumshauri mmiliki namna ya kurekebisha dosari zilizoonekana katika kipindi cha miezi mitatu;

(b) mmiliki ambaye hajatekeleza maelekezo yaliyotolewa na Baraza baada ya miezi mitatu bila kutoa sababu za kufanya hivyo wala kuomba muda wa nyongeza atakuwa ametenda kosa dhidi ya Kanuni hizi na Baraza linaweza kusitisha utambuzi wake kwa muda hadi dosari zitakaporekebishwa.

Utaratibu katika kufuatilia mafunzo

15.Ofisa wa Baraza au mtaalamu aliyeidhinishwa na Baraza anaweza kufuatilia ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni kwa kutumia utaratibu ufuatao:

(a) kutembelea vituo vya kufundishia Kiswahili ambapo Baraza halitalazimika kumjulisha mmiliki kabla ya ziara hiyo;

(b) kuzungumza na wanafunzi waliopo au waliowahi kupata mafunzo kituoni hapo ana kwa ana au kupitia madodoso ili kupata maoni yao;

(c) kuitisha kikao na wamiliki au watumishi wa kituo ili kujadili na kuweka maazimio kuhusu mambo

muhimu yanayojitokeza katika ufundishaji kwenye kituo hicho.

## SURA YA TANO
## MATAMASHA NA MASHINDANO YA KISWAHILI

Baraza kusimamia na kutoa Idhini ya matamasha au mashindano yanayohusisha Kiswahili

16.-(1) Baraza litasimamia matamasha pamoja na mashindano yanayoendeshwa na wadau mbalimbali, yanayohusisha Kiswahili ili kuhakikisha matumizi ya Kiswahili yanakuwa fasaha na sanifu wakati wote wa shughuli hizo.

(2) Mtu, kikundi cha watu, chama cha kitaaluma au asasi yoyote inayokusudia kuendesha tamasha au shindano linalohusisha Kiswahili italazimika kuomba idhini kutoka Baraza kabla ya kuandaa tamasha au shindano hilo.

(3) Matamasha au mashindano yanayolengwa na kanuni hii ni yale ambayo msingi wa ushindani wake ni kuhamasisha au kukuza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu.

(4) Mashindano yoyote yanayohusisha mambo yafuatayo:

(a) nyimbo;
(b) ngonjera;
(c) mashairi;
(d) maigizo;
(e) hadithi;
(f) ucheshi;
(g) uandishi au usomaji wa insha;
(h) uandishi au usomaji wa makala za habari kwa kiswahili;
(i) uandishi au usomaji wa simulizi kwa kiswahili;
(j) uandishi na usomaji wa vitabu kwa kiswahili,

yatahitaji kutambuliwa na baraza kabla ya kufanyika.

Maombi ya idhini ya kufanya matamasha au mashindano

17.-(1) Mwombaji wa Idhini ya tamasha au shindano chini ya Kanuni hizi atafuata utaratibu ufuatao:

(a) atajaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano kwenye Kanuni hizi;
(b) atalipa Tozo ya fomu ya maombi ya idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi;
(c) atawasilisha fomu ikiwa na viambatisho

vilivyotajwa katika fomu hiyo kwa namna atakayoelekezwa wakati wa kuchukua fomu;

(d) mwombaji atajulishwa kuhusu maombi yake mara baada ya Baraza kufanya uamuzi;

(e) mwombaji aliyekubaliwa atajulishwa ili akachukuwe idhini hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Sita katika Kanuni hizi; na

(f) mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa atajulishwa sababu za kukataliwa kwa maombi yake.

(2) Mwombaji aliyekataliwa anaweza kujaza tena maombi ya idhini baada ya kurekebisha dosari zilizobainishwa katika barua ya majibu.

(3) Idhini iliyotolewa chini ya Kanuni hii itatumika kwa ajili ya tukio moja tu na endapo mwombaji anataka kuhuisha idhini au kufanya matukio zaidi ya moja au katika sehemu zaidi ya moja atapaswa kuomba na kulipia idhini kwa kila tukio na kila sehemu anayokusudia kufanya kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Saba.

Usalama wakati wa Tamasha au mashindano

18. Mtu, Kikundi cha watu, chama cha kitaaluma au asasi yoyote iliyopewa Idhini ya kuendesha tamasha au mashindano yoyote chini ya Kanuni hizi itabeba dhamana ya kuhakikisha usalama wa watu na mali zao wakati wote wa shughuli hiyo.

Masharti kabla ya kupewa Idhini

19. Mwandaaji wa mashindano yanayohusisha Kiswahili hatapewa Idhini ya kuendesha tamasha isipokuwa tu kama ameambatisha vitu vifuatavyo:

(a) rasimu ya kanuni zitakazoongoza mashindano hayo;

(b) vigezo vya kupata waamuzi wa mashindano hayo;

(c) wasifu wa waamuzi watakaotumika katika mashindano hayo;

(d) vigezo vya ushindi;

(e) aina ya zawadi zitakazotolewa kwa washindi; na

(f) utaratibu wa makabidhiano ya zawadi kwa washindi.

## SEHEMU YA SITA
## HUDUMA ZA BARAZA KWA VYOMBO VINGINE

*(a) Sekta ya Sanaa na Filamu*

Baraza kuhamasisha na kuelimisha matumizi sahihi ya Kiswahili

20.-(1) Baraza litashirikiana na taasisi yoyote ya umma au asasi binafsi zinazoshughulika na Sanaa au Filamu katika kuelimisha na kuhamasisha watendaji wa sekta ya sanaa na umma kwa ujumla kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili.

(2) Baraza kwa kushirikiana na wadau wengine wa lugha na Sanaa litaendesha semina za kutoa mafunzo kwa watendaji wa sanaa mbalimbali na filamu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutumia Kiswahili fasaha.

Baraza kutoa ushauri

21.-(1) Ikiwa kutajitokeza matumizi ya Kiswahili yasiyozingatia utamaduni wa Tanzania wala staha katika nyimbo, sinema, ngonjera, mashairi au sanaa ya aina yoyote inayotumia maneno ya Kiswahili, Baraza linaweza kutoa ushauri kwa mamlaka yoyote yenye dhamana ya kusimamia na kulinda maadili, heshima na utu wa Mtanzania.

(2) Katika kutekeleza sehemu ya (1) Baraza linaweza kuandika barua na kubainisha:

(a) lugha iliyotumika kimakosa;
(b) athari mbaya zinazoweza kutokana na matumizi ya maneno ya aina hiyo endapo yataachiwa yafike kwenye jamii; na
(c) marekebisho yanayohitajika ili kuepusha athari hizo.

Utaratibu wa kupata tafsiri kutoka Baraza

22.Endapo mamlaka au asasi yoyote inayosimamia au kuratibu sanaa au filamu hapa nchini itatilia shaka Kiswahili kilichotumika katika kazi yoyote iliyoletwa mbele yake; au, endapo kutajitokeza hali ya kutoelewana kuhusu tafsiri ya neno lolote la Kiswahili baina ya vyombo hivyo na msanii au umma, mamlaka au asasi hiyo inaweza kuomba tafsiri rasmi kutoka Baraza na utaratibu ufuatao utatumika:

(a) mamlaka au asasi itaandika barua kwenda Baraza ikiambatisha kazi ya Sanaa yenye tafsiri inayotia shaka, ili kuomba ufafanuzi na ushauri wa kitaalamu kuhusu tafsiri husika;
(b) Baraza litapitia kazi ya sanaa inayohusika na kutoa tafsri rasmi ya neno au maneno husika,

sambamba na kueleza madhara ya maneno husika;

(c) Baraza litapeleka maelezo ya tafsiri rasmi iliyotolewa pamoja na ushauri wa kitaalamu kwa mamlaka au asasi husika; na

(d) mamlaka au asasi husika itafanya uamuzi stahiki kutokana na tafsiri na ushauri uliotolewa na Baraza.

Baraza kuhariri miswada ya kazi za sanaa

23.-(1) Mtu, kikundi, chama cha kitaaluma au asasi yoyote iliyoandika Muswada wa wimbo, mchezo wa kuigiza au kazi nyingine yoyote ya sanaa inayotumia maandishi ya Kiswahili inaweza kupeleka Muswada wa kazi hiyo Baraza au kwa mtaalamu aliyetambuliwa na Baraza kwa ajili ya kuhariri na kuhakiki ufasaha wa Kiswahili kilichotumika kabla ya kupeleka Muswada huo kwenye mamlaka husika.

(2) Mtu au asasi inayopeleka kazi ya sanaa katika Baraza kwa mujibu wa kanuni hii itapaswa kulipa Tozo ya huduma ya uhariri au uhakiki kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

*(b) Sekta ya Habari na Mawasiliano*

Kuimarisha Uhariri katika vyombo vya habari

24. Baraza litashirikiana na mamlaka zingine zinazohusika na kusimamia au kuratibu masuala mbalimbali yanayohusu uandishi wa magazeti au majarida na utangazaji wa maudhui yanayorushwa kupitia redio au runinga kwa kutumia Kiswahili katika kuhakikisha kuwa uandishi na utangazaji katika vyombo husika unafanyika kwa kutumia Kiswahili sanifu na fasaha.

Utaratibu wa kupata tafsiri rasmi

25.-(1) Baraza linaweza kutumika katika kuandaa tafsiri rasmi ya habari au makala iliyorushwa au kuandikwa katika chombo cha habari kwa lugha ya kigeni ili kuitumia katika masuala mengine au kuiwasilisha habari au makala hiyo kwa umma kwa Kiswahili.

(2) Chombo chochote cha habari, mtu binafsi au asasi nyingine yoyote inapohitaji kupata tafsiri rasmi ya Kiswahili kutokana na makala za habari zilizoandikwa au kutangazwa kwa lugha ya kigeni inaweza kupata tafsiri hiyo kutoka Baraza pekee kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) chombo husika kitawasilisha maombi katika Baraza au kwa mtaalamu aliyetambuliwa na

Baraza kwa ajili hiyo na kuambatisha nakala moja ya habari au makala inayopaswa kutolewa tafsiri;

(b) chombo husika kitalipa Tozo ya huduma ya tafsiri rasmi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi; na

(c) mtu binafsi, asasi za kiraia au taasisi yoyote ya Serikali inaweza kufuata utaratibu ulioainishwa katika kanuni hii ili kupata tafsiri rasmi au ufafanuzi kuhusu maana ya neno, kifungu cha maneno au andiko ambalo maana yake ina utata hata kama matumizi yake hayagusi sekta ya habari.

Mafunzo maalumu kwa wanahabari

26.-(1) Baraza litashirikiana na wadau wengine wa sekta ya habari kutoa mafunzo maalumu ya muda mfupi ili kuwajengea waandishi, wahariri na watangazaji walio katika vyombo vya habari na wanaojitegemea uwezo wa kuelewa na kutumia Kiswahili fasaha na sanifu wanapofanya kazi zao.

(2) Ili kufanikisha kipengele cha (1) Baraza:

(a) litashauri wamiliki wa vyombo vya habari kutenga muda na rasilimali muhimu kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa mafunzo hayo;

(b) litaandaa mada na wakufunzi watakaotoa mafunzo husika;

(c) litatoa Cheti cha Mahudhurio kwa kila aliyeshiriki mafunzo hayo.

Baraza kusahihisha makosa ya lugha katika vyombo vya habari

27.-(1) Baraza litakuwa na dhamana ya kuwasiliana na chombo chochote cha habari na kukipa ushauri endapo chombo hicho kimetangaza au kuandika habari zinazopotosha umma kwa kutumia vibaya lugha ya Kiswahili.

(2) Chombo cha Habari kilichopewa ushauri na Baraza kinaweza kutangaza tena habari hiyo kwa usahihi au kutoa ufafanuzi kwa namna nyingine kitakayoona inafaa, ili kuondoa dhana iliyokosewa katika maudhui yaliyotangazwa awali.

(3) Endapo chombo cha habari hakitazingatia marekebisho yaliyoshauriwa, kikaamua kuendelea na upotoshaji, Baraza linaweza kuzitaarifu mamlaka zingine zinazohusika na usimamizi au udhibiti wa maudhui ya kiuandishi au kiutangazaji kwa ajili ya hatua stahiki.

Matangazo ya biashara

28.-(1) Mtu au asasi inayoandaa tangazo la biashara

kuhakikiwa

au la huduma kwa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kurushwa kwa umma kupitia redio, runinga au magazeti, itapeleka rasimu ya tangazo lake Baraza au kwa mtaalamu wa Kiswahili aliyeidhinishwa na Baraza, kwa ajili ya kuhakiki ufasaha na staha ya lugha katika tangazo hilo kabla halijarushwa au kubandikwa hadharani.

(2) Baraza litatekeleza wajibu wake katika kipengele (1) bila kuathiri sanaa au ubunifu uliokusudiwa mahususi kwa kuongeza mvuto usio athiri maadili ya lugha katika kuwasilisha ujumbe uliomo kwenye tangazo husika.

(3) Endapo Kiswahili kilichotumika katika tangazo hilo siyo fasaha, sanifu au hakina staha kiasi kwamba kinaweza kupotosha au kuathiri maadili katika jamii ya watumiaji wa Kiswahili, Baraza linaweza kuzishauri mamlaka husika kuhusu kuwapo kwa dosari na namna ya kuondoa dosari hizo katika tangazo husika.

(4) Endapo tangazo lenye dosari limebandikwa katika bango kwenye eneo la umma Baraza litaishauri Halmashauri husika pamoja na mamlaka zingine zinazohusika kuliondoa au kulisahihisha ili kuepuka upotoshwaji unaotokana na tangazo hilo kuwapo katika eneo husika.

(5) Tangazo lolote lililohakikiwa na Baraza kwa ajili ya kurushwa hewani au kubandikwa katika bango litapewa cheti cha ithibati.

(6) Kurusha au kubandika tangazo bila ya kuwa na cheti cha ithibati kutoka Baraza ni kosa na ikibainika kuwa lugha ya tangazo husika ina dosari na lilibandikwa bila kuhakikiwa, Baraza litazitaarifu mamlaka husika ambazo zinaweza kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.

(7) Chombo cha habari au kampuni ya matangazo italipia Tozo ya uhakiki au uhariri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

(8) Baraza litaweka maofisa au wataalamu waliothibitishwa kufanya uhariri na uhakiki wa Kiswahili katika maeneo ya mikoa na wilaya kwa idadi itakayohitajika kulingana na wingi wa mahitaji ili kuepuka ucheleweshaji wa huduma inayotolewa katika Kanuni hizi.

Matangazo ya dharura au maafa

29.-(1) Tangazo lolote linalokusudiwa kurushwa katika redio au runinga, au kuchapishwa katika gazeti, au kubandikwa katika maeneo ya umma kwa ajili ya kuonya, kukataza au kutahadharisha umma kuhusu hatari yoyote dhidi ya binadamu, mazingira, mifugo au mali zingine za watu au umma, linaweza kuhakikiwa na Baraza au mtaalamu

aliyethibitishwa na Baraza bila malipo yoyote, isipokuwa.

(2) Mtu au asasi yoyote inayohusika na tangazo hilo itaandika kwa Katibu Mtendaji wa Baraza kuomba tangazo hilo lihaririwe au lihakikiwe kama tangazo la dharura au maafa.

(a) Katibu Mtendaji akiona tangazo hilo ni kwa maslahi ya kijamii au kwa sababu nyingine atakayoona inafaa, ataelekeza tangazo hilo kuhaririwa au kuhakikiwa pasipo Tozo;

(b) Endapo Katibu wa Baraza ataona tangazo hilo halina vigezo vilivyotajwa ataelekeza mmiliki alipe Tozo husika kama iliyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

## SEHEMU YA SABA
## HUDUMA ZA BARAZA KWA UMMA

Utaratibu wa kupata huduma na ushauri kutoka Baraza

30. Mtu binafsi, asasi, vyama au taasisi za serikali zinaweza kupata huduma na ushauri katika mambo mbalimbali yanayohusu matumizi ya Kiswahili Kwa kumwandikia Katibu wa Baraza na kubainisha jambo linalohitaji ushauri au kufika na kufanya mazungumzo ya ana kwa ana na maofisa wa Baraza.

Huduma zinazotolewa na Baraza

31.-(1) Baraza kwa kutumia maofisa wake au wataalamu wengine wa Kiswahili waliotambuliwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika Kanuni hizi linaweza kutoa huduma zifuatazo:

(a) kuhariri nyaraka za aina mbalimbali zinazoandaliwa kwa Kiswahili;

(b) kutoa Ithibati katika maandiko au machapisho mbalimbali;

(c) kutafsiri nyaraka na machapisho kwenda au kuja kwenye Kiswahili;

(d) kukalimani lugha mbalimbali kwenda au kuja kwenye Kiswahili;

(e) kufundisha kada mahususi kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili katika uandishi wa nyaraka mbalimbali zinazoandaliwa kwa Kiswahili;

(f) kusaidia watu, vikundi, vyama au asasi zinazofanya tafiti zinazohusisha Kiswahili;

(g) jambo jingine lolote ambalo linahusisha utaalamu

mahususi katika Kiswahili.

(2) Wataalamu waliothibitishwa na Baraza kutoa huduma zilizotajwa katika kipengele cha (1) au jambo jingine lolote kwa mujibu wa Kanuni hizi watakuwa na mamlaka, wajibu au dhamana juu ya jambo hilo kadiri ya kiwango kilichokasimiwa kwao na Baraza.

*(a) Uhariri, tafsiri, uhakiki na ithibati*

Utaratibu wa kupata huduma za uhariri, tafsiri, kuhakiki na kutoa ithibati

32.-(1) Baraza au wataalamu waliothibitishwa na Baraza watatoa huduma za kuhariri, kutafsiri, kuhakiki na kutoa ithibati kutoa ithibati nyaraka na machapisho mbalimbali yaliyoandaliwa kwa Kiswahili ili kuhakikisha zimekidhi viwango vya Kiswahili Sanifu na fasaha kabla hazijatolewa kwa ajili ya matumizi ya umma.

(2) Ili kupata huduma ya uhariri, kutafsiri, kuhakiki na kutoa ithibati utaratibu ufuatao utatumika:

(a) kuwasilisha maombi ya maandishi kwa Katibu Mtendaji wa Baraza yanayobainisha aina ya huduma anayohitaji;
(b) kupewa tathmini ya rasilimali na gharama zinazohitajika katika kupata huduma hiyo;
(c) kulipa Tozo ya huduma hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi;

*(b) Ukalimani wa lugha za kigeni*

Utaratibu wa kupata huduma ya ukalimani wa lugha za kigeni

33.-(1) Baraza linaweza kutumika katika kuratibu au kutoa wakalimani au wafasiri wa nyaraka zitakazohusika katika mikutano mbalimbali inayofanyika nchini au nje ya nchi kwa kuhusisha Kiswahili kama lugha mojawapo ya mkutano huo.

(2) Baraza linaweza kutekeleza jukumu lililotajwa katika (1) kwa kutumia wataalamu walioajiriwa au waliotambuliwa na Baraza kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(3) Mtu, kikundi, chama cha kitaaluma, taasisi ya umma au asasi yoyote inapohitaji huduma ya ukalimani chini ya kanuni hizi itafuata utaratibu ufuatao:

(a) kuwasilisha maombi kwa Katibu Mtendaji wa Baraza kwa njia ya barua ya kawaida au barua pepe yakibainisha aina ya lugha inayohitaji kufanyiwa ukalimani;
(b) Baraza litapeleka mkalimani kutoa huduma

kulingana na mahitaji na itifaki ya shughuli husika; na

(c) mwombaji atalipa Tozo ya maombi ya huduma ya ukalimani wa lugha ya kigeni kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

*(c) Ukalimani wa Lugha ya Alama*

Baraza kusimamia ukalimani wa lugha ya alama

34.-(1) Mara baada ya kutangazwa kwa Kanuni hizi Baraza litaratibu masuala yanayohusu huduma ya ukalimani wa lugha za alama na linaweza kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali au sekta binafsi kadiri litakavyoona inafaa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma ya ukalimani wa lugha ya alama katika shughuli za umma.

(2) Bila kuathiri kanuni na sheria zingine za nchi kuhusu matumizi ya Lugha za alama, Baraza linaweza kufuatilia utoaji na ufasaha wa tafsiri ya lugha hizo katika vituo vya runinga na kuhakikisha kwamba mmiliki wa kituo cha runinga anaweka wakalimani wa lugha za alama katika matangazo yenye tarifa maalumu kwa umma kwa kuzingatia sifa, vigezo na weledi.

(3) Baraza linaweza kushirikiana na wadau wengine wa lugha kuandaa mafunzo mbalimbali mafupi ya ukalimani wa lugha za alama ili kukuza uelewa wa jamii na kuimarisha uwezo wa wataalamu wa ukalimani wa lugha hiyo na wahitimu watatambuliwa na kuingizwa katika kanzidata ya Baraza.

Kanzidata ya wakalimani na wataalamu wa lugha za alama

35.-(1) Tangu tarehe ya kutangazwa kwa Kanuni hizi wataalamu wa lugha za alama watatambuliwa kisha kupewa Idhini ya kuendesha shughuli za ukalimani kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Baraza katika Kanuni hizi na itakuwa ni kosa dhidi ya Kanuni hizi kutoa huduma ya ukalimani wa lugha yoyote ya alama pasipo kutambuliwa na Baraza.

(2) Baraza litatunza kanzidata ya wataalamu hao kwa lengo la kubaini sifa, tabia na uwezo wa kila mtaalamu anayetambuliwa sambamba na kubaini wakalimani wa lugha za alama kwa lugha za kigeni walio katika maeneo mbalimbali nchini ili kusimamia matumizi ya wataalamu hao wanapohitajika katika shughuli za kiraia au za Serikali zinazohusisha umma.

(3) Asasi au mtu yeyote anayehitaji huduma ya ukalimani wa lugha ya alama ana wajibu na haki ya kujua kama mkalimani anayemtumia ametambuliwa na Baraza.

Utaratibu wa kupata mkalimani wa lugha ya alama

36.-(1) Mtu, asasi au taasisi yoyote itakayohitaji kutumia ukalimani wa lugha za alama au huduma nyingine yoyote inayohitaji kufanywa na mkalimani wa lugha ya alama atapaswa kuwasilisha maombi katika Baraza au moja kwa moja kwa mkalimani aliyetambuliwa na kuthibitishwa na Baraza aliye katika eneo husika.

(2) Mtu, taasisi au asasi yoyote inapohitaji mkalimani wa lugha ya alama katika Baraza itafuata utaratibu ufuatao:

(a) itapeleka maombi kwa maandishi kwa Katibu wa Baraza au mkalimani mwenyewe kwa njia ya barua ya kawaida au barua pepe.

(b) Baraza linapopokea maombi ya aina hiyo litapeleka mkalimani kutoka miongoni mwa watumishi wake au litateua mkalimani kutoka miongoni mwa wataalamu walioorodheshwa katika kanzidata ya Baraza.

(3) Asasi au mtu anayeomba huduma hiyo kutoka katika Baraza au kutoka kwa mtaalamu mwingine yeyote aliyetambuliwa na Baraza atalipa Tozo kwa Baraza au kwa mtaalamu aliyethibitishwa na Baraza kwa ajili ya kutoa huduma hiyo kulingana na huduma kwa kuzingatia aina ya shughuli, muda au ukubwa wa hadhira inayohitaji huduma hiyo kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Ishirini katika Kanuni hizi.

## SEHEMU YA NANE
## KISWAHILI KUTUMIKA KAMA BIDHAA

Wajibu wa Baraza katika ubidhaishaji wa Kiswahili

37.-(1) Baraza litahamasisha na inapohitajika litatoa ushauri wa kitaalam kwa mtu, kikundi, chama cha kitaaluma au asasi yoyote iliyotambuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi kutumia Kiswahili kama bidhaa inayoweza kuuzwa na kuingiza kipato.

(2) Mtu hatazuiliwa kutumia Kiswahili kama bidhaa kwa sababu ya kuishi nje ya Tanzania au kutokuwa Mtanzania kama anazo sifa za kutambuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Bidhaa za Kiswahili

38. Bila kuathiri maudhui ya kanuni za 32, 33, 34, 35 na 36 kwenye kanuni hizi, mtu, kikundi au asasi inaweza

kubuni au kuibua shughuli yoyote inayoweza kuitumia kama bidhaa na kuingiza kipato nchini, shughuli zifuatazo zinaweza kuuzwa kama bidhaa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni hizi:

(a) kuhariri maandiko mbalimbali;
(b) kuhakiki matumizi ya maneno;
(c) kutafsiri maandiko mbalimbali;
(d) ukalimani wa lugha mbalimbali;
(e) ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni;
(f) uandishi wa simulizi, ngonjera au mashairi kwa Kiswahili;
(g) kuendesha mashindano au michezo inayoshindanisha maudhui kwa Kiswahili; na
(h) jambo lingine lolote linalohusisha Kiswahili linaloweza kutolewa kama huduma.

Utaratibu wa kupata Idhini ya kutoa huduma zinazohusisha Kiswahili

39.-(1) Mtu, kikundi cha watu au asasi yoyote inayotaka kutoa huduma kwa kutumia bidhaa za Kiswahili zilizotajwa katika kanuni ya 38 italazimika kuomba idhini kutoka Baraza kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) kujaza fomu ya maombi ya Idhini iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza au la Tisa au la Kumi na Mbili kwenye Kanuni hizi, kulingana na aina ya huduma inayotaka kutoa;
(b) kulipa Tozo ya maombi iliyoainishwa katika Jedwali la Ishirini;
(c) kulipa ada ya Idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini na Moja; na
(d) kupatiwa Hati ya idhini kutoka Baraza kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni hizi.

(2) Mtu binafsi, kikundi cha watu, chama au asasi iliyopewa Idhini ya kutoa huduma hapa Tanzania Bara haitazuiwa kutafuta fursa nje ya nchi, na endapo itapata fursa ya kutoa huduma hiyo nje ya Tanzania Bara itapaswa kuliarifu Baraza kwa ajili ya kupata hati ya utambulisho endapo itahitajika katika kutimiza taratibu zingine katika mamlaka husika.

(3) Mtu, asasi au taasisi iliyopata fursa ya kufanya shughuli zinazotumia Kiswahili nje ya Tanzania Bara inapohitaji kutumia wataalamu kutoka Tanzania itapaswa kuwasilisha katika Baraza taarifa zifuatazo:

(a) katiba au andiko linaloonyesha aina ya shughuli anayofanya huko aliko kwa kutumia Kiswahili;
(b) usajili wa asasi anayoitumia kufanyia huduma

anayoitoa kwa mujibu wa sheria na mamlaka za huko aliko;

(c) anwani ya mahali ambapo anafanyia shughuli zake;

(d) aina na idadi ya wataalamu wa Kiswahili anaowahitaji kutoka Tanzania Bara;

(e) muda ambao atahitaji kuwatumia; na

(f) mikataba inayoonyesha stahiki za wataalamu hao kwa kipindi chote atakachowatumia huko ugenini.

(4) Baraza kwa kushirikiana na wadau au mamlaka zingine za Serikali zenye dhamana linaweza kuratibu upatikanaji wa mtaalamu au wataalamu wanaohitajika.

(5) Hati ya Utambuzi inayotolewa na Baraza chini ya kanuni hii itakuwa hai kwa kipindi cha miezi kumi na miwili, na inaweza kuhuishwa kwa:

(a) kujaza fomu mahususi kwa ajili hiyo kama ilivyoainishwa katika Kanuni hizi;

(b) kuambatisha hati ya Idhini ya awali;

(c) kulipa Tozo ya maombi ya kuhuisha idhini husika kama ilivyoanishwa kwenye Jedwali la Ishirini;

(d) kulipa ada ya Idhini mpya kama ilivyo ainishwa katika Jedwali la Ishirini na Moja na kuambatisha stakabadhi za malipo husika.

Ufuatiliaji na tathmini

40. Baraza linaweza kutembelea wadau wanaojishughulisha na huduma za Kiswahili ili kufuatilia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Baraza na kutathmini uendeshaji wa shughuli hizo kama unakuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili.

## SEHEMU YA TISA
## UTAFITI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

Idhini ya utafiti kutolewa na Baraza

41.-(1) Mtu au asasi yoyote inayokusudia kufanya utafiti unaohusu lugha ya Kiswahili hapa Tanzania Bara italazimika kupata idhini ya Baraza baada ya kupata vibali kutoka mamlaka zingine zinazohusika na masuala ya tafiti nchini.

(2) Idhini ya Baraza kwa ajili ya utafiti unaohusu Kiswahili nchini itapatikana kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) kujaza fomu ya kuomba idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Tano na

kurejesha ikiwa na viambatisho vilivyotajwa;

(b) kulipa Tozo ya maombi ya Idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini; na

(c) endapo maombi yamekubaliwa mwombaji atajulishwa ili aweze kulipa ada ya idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini na Moja kwenye kanuni hizi.

(3) Itakuwa ni kosa kwa mtu, asasi au taasisi yoyote ya ndani au nje ya Tanzania Bara kuendesha shughuli za utafiti binafsi wa Kiswahili hapa nchini pasipokuwa na idhini ya kufanya hivyo kutoka Baraza, isipokuwa masharti katika kifungu hiki hayatahusu tafiti za wanafunzi wanaofanya masomo yao ya lugha au utamaduni katika vyuo vikuu vinavyotambulika na Serikali vilivyopo hapa nchini.

(4) Endapo taasisi iliyoomba kufanya utafiti kuhusu Kiswahili inatoka nje ya Tanzania Bara na inahitaji kuzunguka katika sehemu mbalimbali za nchi italazimika kuambatana na mtafiti mkazi kutoka Baraza au taasisi ya utafiti inayotambulika na Baraza.

(5) Idhini inayotolewa chini ya kanuni hii itadumu kwa miezi 12 na mmiliki anaweza kuhuisha kwa:

(a) kujaza fomu mahususi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kumi na Saba;

(b) kulipa Tozo ya maombi ya kuhuisha idhini kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini;

(c) kulipa ada ya idhini mpya kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini na Moja.

Taarifa au takwimu zilizo katika Baraza

42.-(1) Mtu yeyote, asasi, taasisi ya umma au binafsi inaweza kuomba kupatiwa taarifa au takwimu za lugha ya Kiswahili zilizo katika Baraza kwa kuwasilisha barua ya maombi kwa Katibu Mtendaji.

(2) Mtu au asasi inayoomba kupatiwa taarifa au takwimu zilizo katika Baraza itafuata utaratibu ufuatao:

(a) kuandika barua ya maombi kwa Katibu wa Baraza kuelezea pamoja na mambo mengine;

(i) aina ya tarifa zinazoombwa;

(ii) matumizi ya tarifa zinazoombwa.

(b) kulipa Tozo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini kwenye Kanuni hizi.

## SEHEMU YA KUMI
## UANDISHI WA VITABU NA ITHIBATI

Baraza kuhamasisha waandishi chipukizi

43.-(1) Baraza litahamasisha waandishi chipukizi wa vitabu vya Kiswahili kwa kuwapa huduma ya ushauri na uhariri bila malipo ili kukuza uandishi wa vitabu kama njia ya kuhifadhi istilahi na kukuza matumizi ya Kiswahili fasaha.

(2) Baraza linaweza kufanya mambo mbalimbali yanayolenga kuhimiza matumizi ya lugha za kijamii sambamba na kuratibu tafiti mbalimbali zinazohusu lugha hizo, ili kukuza istilahi za Kiswahili kwa ajili ya kuendeleza uandishi bora wa vitabu.

Vitabu vya kiada na ziada kuthibitishwa

44.-(1) Mwandishi yeyote wa kitabu cha kiada au cha ziada kilichoandikwa kwa Kiswahili atapaswa kupeleka mswada wa kitabu chake Baraza ili kupata ithibati ya ufasaha wa lugha iliyotumika kabla ya kukichapisha kwa matumizi yaliyokusudiwa.

(2) Ili kupata ithibati ya kitabu kilichoandikwa kwa Kiswahili mwandishi au mchapishaji wa kitabu hicho atapaswa:

(a) kumwandikia barua Katibu wa Baraza kuomba Ithibati;
(b) kuambatisha muswada wa kitabu kinachoombewa ithibati; na
(c) kulipa Tozo ya ithibati kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Ishirini.

(3) Baraza litatoa ithibati kwa kufuata utaratibu ufuatao:

(a) litapitia muswada uliowasilishwa ili kubaini kama kuna upungufu wowote katika matumizi ya lugha;
(b) endapo kutakuwa na upungufu katika ufasaha wa Kiswahili kilichotumika Baraza litarejesha muswada huo kwa mwandishi au mchapishaji pamoja na maelekezo ya marekebisho;
(c) litahakiki muswada uliowasilishwa mara ya pili ili kuona kama maelekezo yamezingatiwa;
(d) ikiwa marekebisho yamezingatiwa Baraza litatoa cheti cha ithibati kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Nane.

(4) Cheti cha ithibati kitadumu muda wote wa kitabu hicho isipokuwa kama mwandishi atatoa toleo lingine la kitabu hicho.

Kusambaza kitabu kisicho na ithibati

45. Ikithibitika kuwa mwandishi au mchapishaji wa kitabu cha Kiswahili amesambaza kitabu kisicho na ithibati kutokana na ama kutoombewa ithibati au kutozingatiwa kwa marekebisho yaliyoelekezwa, Baraza linaweza kuwasilisha maoni kwa mamlaka zingine zinazoweza kudhibiti madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na usambazaji wa kitabu hicho.

Wahariri binafsi kutumika

46.-(1) Endapo Baraza litabaini kuwa utekelezaji wa Kanuni hizi unaathiriwa na uhaba wa maofisa, Baraza linaweza kutumia wahariri binafsi waliotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi cha Baraza kwa mujibu wa Kanuni hizi ili kuongeza ufanisi na tija.

(2) Mhariri aliyethibitishwa anapomaliza kazi yake atawasilisha taarifa ya tathmini yake akiambatisha na muswada uliotathminiwa kwenda katika Baraza ili cheti cha ithibati kiweze kutolewa.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## KISWAHILI KATIKA BIDHAA NA MAZINGIRA YA VIWANDA

Baraza kufuatilia matumizi ya Kiswahili katika bidhaa za viwandani

47.-(1) Baraza litahamasisha na kufuatilia matumizi ya Kiswahili kwenye bidhaa na vifungashio vya bidhaa.

(2) Baraza linaweza kufanya ziara katika viwanda au maghala yanayotumika kuzalishia au kuhifadhia bidhaa wakati wowote ili kuhakiki utekelezaji wa kanuni hii.

Elimu na Uhamasishaji

48. Katika kuhamasisha na kufuatilia matumizi ya Kiswahili fasaha katika bidhaa, na vifungashio vya bidhaa Baraza litafanya mambo yafuatayo:

(a) kutembelea maeneo ya uzalishaji, uhifadhi na uuzaji wa bidhaa za viwandani ili kuhakiki kama taarifa na maelezo muhimu yanayobandikwa kwenye vifungashio vya bidhaa hizo yameandikwa au kutafsiriwa kwa Kiswahili fasaha;

(b) litashirikiana na mamlaka husika kupima kama tafsiri ya maelezo yaliyobandikwa kwenye bidhaa yanamwezesha mtumiaji wa bidhaa kuelewa matumizi na jinsi ya kutunza au kuandaa bidhaa hiyo kabla ya kutumia;

(c) kuhakiki matumizi ya Kiswahili kwenye mabango ya matangazo na vipeperushi vya maelekezo ya jumla kwa watumiaji kuhusu ubebaji, utunzaji, uandaaji na utumiaji wa bidhaa zinazotengenezwa au kuingizwa nchini.

Wajibu wa kutumia Kiswahili na kutafsiri maelekezo kwenye bidhaa

**49.**-(1) Mtu, asasi au taasisi yoyote inayozalisha, kusambaza au kuingiza nchini bidhaa za viwandani kwa ajili ya matumizi ya umma itahakikisha inabandika maelezo au maelekezo yanayotumia Kiswahili fasaha katika kila bidhaa inayohusika nayo.

(2) Mtu, asasi au taasisi yoyote inayozalisha, kusambaza au kuingiza nchini bidhaa za viwandani ambazo maelekezo yake yako katika lugha za kigeni itawajibika kuhakikisha maelezo hayo yametafsiriwa kwa Kiswahili fasaha ili kumwezesha mlaji kuelewa ipasavyo kuhusu bidhaa hiyo kabla ya kuitumia.

(3) Mtu, kikundi au asasi yoyote inayoingiza au kusambaza bidhaa ambayo maelezo yake ni ya lugha ya kigeni bila ya kufanya tafsiri kwa Kiswahili fasaha itakuwa imekiuka Kanuni hizi na Baraza linaweza kuzitaarifu mamlaka zinazosimamia viwanda au waingizaji wa bidhaa husika kuhusu ukiukwaji huo.

